KANTAR

**Kantar Africa Mashariki**

**SERA YA FARAGHA NA YA VIDAKUZI YA TAFITI** ("Sera")
Mwisho kusasishwa: Septemba 2023

**Utangulizi:**

Tafiti zetu hufanywa na Kantar Africa Mashariki.

Tunafanya utafiti wa masoko kwa niaba ya wateja na mara nyingi, mteja ndiye mshirika anayewajibika (pia anajulikana kama mdhibiti wa data) na sisi tunafanya kazi kama mtendaji (pia anajulikana kama mchakataji wa data).

Tunakuomba usome sera hii ya faragha kwa makini.

Kwa madhumuni ya Sera hii, ufafanuzi wa "maelezo ya binafsi" ni maelezo yanayohusiana na mtu na/au kampuni na yanaweza kumtambulisha (panapohitajika).

**Ukusanyaji na matumizi yanayokubalika kisheria:**

Sera Hii inafafanua jinsi tunavyokusanya, kuhifadhi na kutumia maelezo ya binafsi unayowasilisha unaposhiriki katika utafiti wa mtandaoni, ana kwa ana, kupitia posta au kupitia simu kwa matumizi yetu.

Tunapofanya utafiti, wanaohoji/mialiko/mifumo na dodoso zetu zinatubainisha wazi na zinafafanua madhumuni yetu ya kuwasiliana, na panapohitajika, madhumuni yetu ya kukusanya maelezo yako ya binafsi. Unaweza kukataa kujibu maswali yoyote au ujiondoe ili usishiriki katika utafiti wakati wowote.

Tunapowasiliana nawe, kwa jumla ana kwa ana, kupitia simu, kupitia barua pepe au kupitia posta, tunafanya hivyo ili kutekeleza mojawapo ya madhumuni yafuatayo:

| **Tukio** | **Madhumuni** | **Data inayokusanywa/inayochakatwa** | **Msingi wa Kisheria** |
|---|---|---|---|
| Kukualika ushiriki katika tafiti zetu | Kutoa fursa ili kuruhusu sampuli ya watu washiriki katika tafiti zetu | Nambari ya simu iliyopigwa (kwa nasibu), anwani ya posta, anwani ya barua pepe | Idhini au lengo halali (panapohitajika)<br><br>Tuna lengo halali la kuwasiliana na sampuli ya watu ili kuwaalika washiriki katika tafiti zetu.<br><br>Kantar au mteja wake wanatumia idhini yako ya kuwasiliana nawe ili kukualika ushiriki katika utafiti. |
| Tafiti | Kufahamu maoni yako kuhusu bidhaa na huduma fulani au kufahamu tabia yako katika hali tofauti.<br>Kuthibitisha majibu uliyotoa katika utafiti wa hivi majuzi tuliofanya.<br>Kuwezesha kushiriki, kwa mfano, droo za kushinda zawadi, vichocheo, shughuli za utangulizi na kadhalika.<br>Kuwasiliana upya na washiriki, kwa mfano, katika tafiti zinazoendelea na za ufuatilizi. | Kitambulishi cha kipekee, maelezo ya mawasiliano, anwani ya barua pepe, sauti, picha, maoni | Kushiriki kwa hiari katika utafiti ambapo tunakuomba idhini ya kutumia maelezo yako ya binafsi. |
| Ulinzi Dhidi ya Ulaghai | Ulinzi wa malengo ya biashara yetu dhidi ya tabia ya ulaghai | Anwani ya IP, maelezo ya kivinjari, maelezo ya kifaa, anwani za posta, anwani za barua pepe | Malengo halali – tuna lengo halali la kulinda biashara yetu dhidi ya ulaghai au tabia nyingine isiyoruhusiwa. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Upekee wa Kushiriki<br><br>Katika Utafiti | Kuzuia mtu mmoja asishiriki mara nyingi katika utafiti | Anwani ya IP, maelezo ya kivinjari, maelezo ya kifaa | Malengo halali – tuna lengo halali la kumzuia mtu mmoja ashiriki mara nyingi. |
| Uboreshaji na Ulinganishaji wa Data | Tunaboresha data tunayohifadhi kwenye faili kukuhusu kwa kulinganisha maelezo yako ya binafsi katika vyanzo vingine vya data na washirika wengine wanaotoa huduma ya kudhibiti data. | Kitambulishi cha kipekee, maelezo ya mawasiliano, anwani ya barua pepe, maelezo ya kuingia katika mitandao jamii, vidakuzi, kitambulisho cha kifaa cha mkononi | Kushiriki kwa hiari katika utafiti ambapo tunakuomba idhini ya kutumia maelezo yako ya binafsi. |
| Kudhibiti matukio ya kujiondoa katika utafiti wa simu | Wakati mtu ameomba asipigiwe simu tena, tunahifadhi maelezo yake ili kutimiza ombi hili. | Jina na nambari ya simu | Malengo halali – tuna lengo halali la kuhifadhi maelezo hayo ili kutimiza ombi la mtu huyo. |

Hatutawahi kujiwakilisha vibaya au kuwakilisha tunachofanya kwa njia isiyofaa. Ukipokea barua pepe unayotilia shaka, inayodai kutoka kwetu, tafadhali tujulishe jinsi tulivyoonyesha hapa chini katika sehemu ya “Jinsi ya kuwasiliana nasi”.

Tunawasiliana nawe ili ushiriki katika utafiti kupitia simu, posta, ana kwa ana au mtandaoni kwa

- Kubisha kwenye mlango wako, kwa nasibu
- Kupiga nambari yako kwa kutumia Kipigaji cha Nambari kwa Nasibu (RDD)
- Kupokea maelezo yako ya mawasiliano kutoka kwa mteja tunayemfanyia utafiti, ambaye huenda umejisajili kwake, umepokea bidhaa au huduma kutoka kwake, au mmefanya mambo pamoja kwa jumla
- Kununua sampuli kutoka kwa mtoa huduma za sampuli
- Kutafuta maelezo yako kutoka kwenye nyenzo zinazopatikana hadharani
- Kupokea maelezo yako ya mawasiliano kutoka kwa mwajiri ambaye amekuwa akiwasiliana nawe
- Au ulikubali awali tuwasiliane nawe tena ili ushiriki katika tafiti zaidi ikiwezekana

**Washirika wengine na uhamishaji wa data nje ya mipaka:**

Tunakusanya na kuchakata maelezo ya binafsi kwa madhumuni yaliyofafanuliwa hapa juu, lakini hatushiriki wala kuuza maelezo yako ya binafsi kwa washirika wengine, isipokuwa yahitajike kisheria, au ukubali vinginevyo.

Huenda maelezo yako ya binafsi yakakusanywa, kuhifadhiwa, kuhamishwa au kuchakatwa na kampuni zetu tanzu za Kantar, au watoa huduma wengine kwa madhumuni yanayohusiana na utafiti, kama vile kuchakata data, na kutimiza droo za zawadi au vichocheo vingine ndani na nje ya nchi unakoishi. Washirika wote wana wajibu wa kimkataba wa kuhifadhi kwa siri maelezo yoyote wanayokusanya na kutuonyesha au, tunayokusanya na kuwaonyesha; na ni lazima wayalinde kupitia kanuni na mbinu za usalama ambazo zinafanana na zetu. Iwapo maelezo yako ya binafsi yamehamishiwa, kuhifadhiwa, au kuchakatwa vinginevyo katika eneo lililo nje ya nchi unakoishi (panapohitajika) na eneo hilo halijatambuliwa kutoa ulinzi wa maelezo ya binafsi kwa njia ya kutosha, tutaweka ulinzi unaofaa kisheria. Kwa mfano, vifungu rasmi vya mkataba na mamlaka mengine yanayofaa, yanayofanya kazi na washirika ambao wanatumia sheria rasmi za kampuni au michakato mingine kati ya vikundi, wanaoomba idhini yako ili kuhamisha maelezo ya binafsi, ambapo uhamishaji unahitajika katika utendaji wa mkataba kati yetu au ambapo mkataba uliwekwa kwa niaba yako, au ambapo uhamishaji unahitajika ili kubaini, kutekeleza au kutetea madai ya kisheria.

KANTAR

**Usiri, usalama na mahitaji ya kisekta:**

Tumeweka mikakati inayofaa ya kiteknolojia na kimashirika ili kulinda maelezo yako ya binafsi na kuchukua hatua zote zinazofaa ili kuhakikisha kuwa maelezo yako ya binafsi yanachakatwa kwa njia salama. Maelezo yote unayotupa huhifadhiwa katika seva na mazingira salama. Kwa bahati mbaya, hamna uhamishaji wa data unaoweza kuwa salama kwa asilimia 100. Kwa sababu hiyo, ingawa tunajitahidi kulinda maelezo yako ya binafsi, hatuwezi kuhakikisha usalama wa maelezo yoyote unayotutumia au yanayotoka kwenye bidhaa au huduma zetu za mtandaoni, na utawajibikia matendo yako. Pindi tunapopokea maelezo yako, tutachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kuwa mifumo yetu ni salama.

Wakandarasi wetu wanaotoka kwingine, watoa huduma walio katika eneo na wafanyakazi wetu wana wajibu wa kimkataba wa kufuata sera na taratibu zetu zinazohusu usiri, usalama na faragha.

Tunatimiza mahitaji yafuatayo ya kisekta:

- GDPR, Sheria ya Uingereza ya 2018 ya Ulinzi wa Data, GDPR ya Umoja wa Ulaya, Sheria ya 4 ya 2013 ya Ulinzi wa Maelezo ya Binafsi, sheria zozote zinazotumika nchini za ulinzi wa data na sheria zozote zinazohusika, ambazo zinaweza kubadilishwa baada ya muda fulani.
- Tunafuata Kanuni za Maadili za MRS na ESOMAR.

Tunajumuisha majibu yako ya utafiti katika utafiti fulani na majibu ya wengine wote wanaoshiriki, na kuripoti majibu hayo yaliyojumuishwa kwa mteja aliyeomba utafiti, isipokuwa kigezo kimoja au zaidi kati ya vifuatavyo vitimizwe.

Hali za kipekee zinazoweza kufanya tufichue maelezo yako ya binafsi au majibu ya utafiti kwa washirika wengine kama zifuatazo:

- Uombe au ukubali tushiriki maelezo yanayokutambulisha na/au majibu ya kibinafsi na mshirika mwingine kwa madhumuni mahususi.
- Tunapotuma majibu yako kwa mchakataji mwingine ambaye ana wajibu wa kimkataba wa kuhifadhi kwa siri maelezo hayo na kuyatumia tu kwa madhumuni ya utafiti au ya takwimu.

**Ufichuzi wa vidakuzi (kwa wanaoshiriki tu katika utafiti wa mtandaoni):**

Vidakuzi ni faili ndogo za maandishi zinazohifadhiwa kwenye kompyuta au kifaa chako na tovuti ambayo hukipa kitambulisho cha nambari ya mtumiaji na huhifadhi maelezo fulani kuhusu jinsi unavyovinjari mtandaoni. Vinatumiwa na wasanidi wa wavuti ili kuwasaidia watu watumie tovuti zao kwa njia bora na kutekeleza shughuli fulani. Tovuti hutuma maelezo kwenye kivinjari ambacho huunda faili ya maandishi. Kila mara mtumiaji anaporudi kwenye tovuti hiyo, kivinjari hicho hutafuta na kutuma faili hii kwenye seva ya tovuti husika.

Hatutumii vidakuzi kwenye tafiti rasmi za mtandaoni za ndani ya kampuni. Iwapo vidakuzi vinahitajika na mfumo wa mshirika, taarifa hizi hutolewa na sera au ilani ya faragha ya mfumo husika.

Kwa tafiti za kufuatilia tabia, tunatumia programu au vidakuzi vya hiari, lakini iwapo tu umetoa idhini dhahiri kwa vidakuzi au programu hizo.

Jinsi ilivyo katika tafiti nyingi za mtandaoni, tunakusanya taarifa fulani kiotomatiki na kuzihifadhi katika faili za data ya utafiti. Maelezo haya yanaweza kujumuisha mambo kama vile anwani ya Itifaki ya Intaneti (anwani ya IP), aina ya kivinjari, Mtoa Huduma za Intaneti (ISP); kurasa za kurejelea au za kufunga, mfumo wa uendeshaji na muhuri wa tarehe au wa wakati.

Tunatumia maelezo haya yaliyokusanywa kiotomatiki ili kuchanganua mitindo kama vile matumizi ya kivinjari na kusimamia tovuti, kwa mfano, kuboresha hali ya utafiti kulingana na aina ya kivinjari chako. Tunaweza pia kutumia anwani yako ya IP kukagua iwapo umeshiriki mara nyingi katika utafiti ukitumia anwani hii ya IP.

**Usahihi:**

Tunachukua hatua zote zinazowezekana ili kuhifadhi maelezo yako ya binafsi kwa njia sahihi, kamilifu, faafu na kuyasasisha, kulingana na maelezo mapya zaidi unayotupatia. Iwapo ungependa kusasisha maelezo yako ya binafsi, tafadhali wasiliana nasi ukitumia maelezo tuliyoweka hapa chini.

Tunakutegemea ili utusaidie kuhifadhi maelezo yako ya binafsi kwa njia sahihi, kamilifu, na kuyasasisha kwa kujibu maswali yetu kwa njia ya kweli na una wajibu wa kuhakikisha kuwa mshirika anayehusika (ambaye anaweza kuwa sisi au – mteja wetu – mara nyingi) anaarifiwa kuhusu masasisho au mabadiliko yoyote kwenye maelezo yako ya binafsi.

**Kukusanya data ya watoto:**

Huwa hatualiki kimakusudi watoto walio na umri wa chini ya miaka 18 kushiriki katika tafiti bila idhini. Iwapo inahitajika na inafaa watoto washiriki katika mradi fulani unaohusisha watoto walio na umri wa chini ya miaka 18, tunachukua hatua ili kuhakikisha kuwa tumepewa ruhusa na mtu mzima anayehusika. Hatuuzi maelezo ya binafsi ya watoto.

**Kukusanya maelezo maalum**

Katika utafiti wetu tunaweza kuomba kukusanya maelezo ya binafsi ambayo yamebainishwa kama “aina maalum” ya maelezo ya binafsi. Maelezo haya yanajumuisha chanzo cha mbari au kabila, maoni ya kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, au uanachama kwenye miungano ya wafanyakazi, data ya kijenetiki, data ya bayometriki kwa madhumuni ya kutambua mtu kwa njia ya kipekee, data inayohusu afya au data inayohusu maisha ya kingono au mwelekeo wa kingono wa mtu halisi. Utaweza kila wakati kuchagua iwapo utatupatia data hii ili itumiwe jinsi ilivyofafanuliwa.

**Haki za watu:**

Ili uombe idhini ya kufikia maelezo ya binafsi tunayohifadhi kukuhusu, unapaswa kutuma ombi lako kwa kuandika kwa anwani ya barua pepe au anwani ya posta iliyoonyeshwa hapa chini katika sehemu ya “Jinsi ya Kuwasiliana Nasi”. Unapotuma ombi, unapaswa kuashiria kitengo cha Kantar ambako unatuma ombi (na, kwa mfano, kitambulisho chako cha jopo au kitambulishi kingine).

Iwapo utawasiliana nasi ukitumia anwani ya barua pepe au maelezo ya mawasiliano ambayo hatujahifadhi, utahitaji pia kuweka nakala ya kitambulisho halali kilichotolewa na serikali au hati rasmi (kama vile pasipoti au leseni ya udereva).

Una haki zifuatazo kwa mujibu wa maelezo yako ya binafsi:

- Haki ya kubadilisha uamuzi na kuondoa idhini yako
- Haki ya kufikia maelezo yako ya binafsi
- Haki ya kubadilisha maelezo yako ya binafsi
- Haki ya kufuta maelezo yako ya binafsi kwenye mifumo yetu, isipokuwa tuwe na sababu halali za kuendelea kuchakata maelezo hayo
- Haki ya kuhamisha maelezo yako ya binafsi (haki ya uhamishaji)

- Haki ya kuzuia uchakataji wa maelezo yako ya binafsi
- Haki ya kupinga uchakataji wa maelezo yako ya binafsi
- Haki ya kutobaguliwa kwa kutumia haki zozote ulizonazo kwa mujibu wa sheria za ulinzi wa data zinazotumika

Ikihitajika, tutaarifu washirika wengine wowote kama vile wauzaji au watoa huduma wetu ambao tumewatumia maelezo yako ya binafsi kuhusu mabadiliko yoyote tunayofanya unapotuma ombi. Kumbuka kuwa ingawa tutawasiliana na washirika hawa wengine, hatuwajibikii hatua wanazochukua ili kujibu ombi lako. Huenda ukaweza kufikia maelezo yako ya binafsi yanayohifadhiwa na washirika hawa wengine na kurekebisha, kubadilisha au kufuta maelezo hayo iwapo si sahihi.

**Kuhifadhi na kudumisha data:**

Maelezo ya binafsi yatahifadhiwa tu kwa kipindi kinachofaa kwa matumizi yanayonuiwa na ya kisheria; katika hali hii hatutahifadhi data kwa zaidi ya miezi 12, isipokuwa ihitajike kisheria kufanya hivyo. Maelezo ya binafsi ambayo hayahitajiki yatafutwa katika njia ambazo zitadumisha usiri.

Kama sehemu ya mpango wa Uendelevu wa Biashara ya Kampuni na kwa mujibu wa uthibitishaji wa ISO 27001, ISO 9001, ISO 20252 panapohitajika, na katika matukio fulani ya kisheria, nakala kwenye mifumo yetu ya kielektroniki huhifadhiwa na kuwekwa katika kumbukumbu. Kumbukumbu hizi huhifadhiwa kwa kipindi fulani katika mazingira yanayodhibitiwa kikamilifu. Baada ya muda huo kuisha, data hufutwa na kifaa halisi huharibiwa ili kuhakikisha kuwa data imefutwa kikamilifu.

**Arifa kuhusu mabadiliko muhimu**

Tunakagua sera yetu ya faragha mara kwa mara, na inaweza kubadilishwa kadri muda unavyosonga. Kila mara tutakuwa na sera mpya zaidi kwenye ukurasa huu wa wavuti. Tutaandika mara ya mwisho ambapo sera ilibadilishwa.

Tarehe ya kutungwa: 13/06/2011
Mwisho kubadilishwa: 11/09/2023

**Kufanya uamuzi au uainishaji wa kiotomatiki:**

Katika hali fulani tutafanya uamuzi au uainishaji wa kiotomatiki kukuhusu. Hata hivyo, katika hali nyingi hatua hii haitasababisha maamuzi yoyote yenye athari kubwa za kisheria kufanywa kukuhusu. Una haki ya kukata rufaa iwapo uamuzi wowote uliofanywa kiotomatiki kukuhusu una athari kubwa ya kisheria. Iwapo una maswali yoyote kuhusu hili, tafadhali wasiliana nasi.

**Jinsi ya kuwasiliana nasi:**

Iwapo hujafurahia jinsi tulivyochakata maelezo yako ya binafsi, tungependa utupe nafasi ya kurekebisha. Unaweza kuwasiliana nasi kupitia Privacyweca@Kantar.com. Unaweza pia kuwasiliana na Afisa wetu wa Ulinzi wa Data, Evelyne Bosibori, kupitia Evelyne.Bosibori@Kantar.com. Afisa wetu wa Ulinzi wa Data hufuatilia jinsi tunavyotii Sheria za Ulinzi wa Data pamoja na sera yetu ya faragha na ni mwakilishi wetu wa mamlaka za usimamizi kuhusu masuala yanayohusiana na kuchakata maelezo ya binafsi.

**Malalamiko na ufumbuzi katika nchi mahususi:**

Iwapo hujafurahia jinsi tulivyochakata maelezo yako ya binafsi, tungependa utupe nafasi ya kurekebisha. Tafadhali wasiliana nasi kupitia info@kantar.com na mmoja wetu atawasiliana nawe. Hata hivyo, una haki ya kuwasilisha malalamiko kwenye mamlaka ya usimamizi kama vile Mdhibiti wa Ulinzi wa Data au Mdhibiti wa Maelezo katika nchi yako.

Sisi ni Kantar Group Company. Jina na anwani yetu iliyosajiliwa ni Kantar TNS RMS East Africa & Millward Brown East Africa Limited, The Templeton, Matundu Lane, Westland's PO Box 72951-00200, Nairobi, Kenya.